KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 10, Issue 2

10th Jumâ dal-Aakhir 1432

13th May, 2011

YALIYOMO

Makosa Arubaini Yanayohusiana Na Swala 1 - 4

MAKOSA ARUBAINI YANAYOHUSIANA NA SWALA

Sheikh Saalih Ibn Abdul-Azeez Ibn Muhammad Aali-Shaykh

1. KUWACHA SWALA KABISA.

Hakika hili ni jambo la kufru (ukafiri) na ushahidi wapatikana ndani ya Qur'an, Sunnah swaheeh na maafikiano ya Ummah (Ijmaa'). Allaah (سبحانه وتعالى) amesema: **"Kama wakitubu na wakasimamisha swala na wakatoa zaka, basi ni ndugu zenu katika dini."** [at-Tawbah-9:11]

Na amesema: **"Ni kipi kilichokupelekeni motoni? Waseme: "Hatukuwa miongoni mwa waliokuwa wakiswali."** [al-Insaan 74:42-43] na kadhaalika

Na katika Sunnah, hadeeth ya Jaabir (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Baina ya mtu na shirk (kinachomuhifadhi na shirk) ni kuacha swala [Muslim].

Imepokewa na [Abu Dawood, An-Nasaa'i, Ibn Maajah, na At-Tirmidhi Ahmad] na wengineo na ni swaheeh - kutoka kwa Buraidah Ibn Al-Husaib (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Mkataba baina yetu na wao (Mtume pamoja na wafuasi wake na wenye kudai kuwa ni Waislamu) ni swala, kwahivyo yoyote atakaewacha amekufuru." Ama kuhusu Ijmaa', Abdullah ibn Shaqeeq (رضي الله عنه) amesema: Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) hawakuona kuwaacha kitendo kingine kuwa ni kufru ila kuacha swala [at-Tirmidhi na wengineo kwa isnad swaheeh]

2 KUICHELEWESHA SWALA KUTOKA KWENYE WAKATI WAKE ULIOWEKWA.

Huku ni kukiuka mipaka kulingana na neno la Allaah (سبحانه وتعالى): **"Kwa hakika swala kwa Waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati makhsusi."** [an-Nisaa-4:103] Al-Mawqoot ina-ashiriya nyakati maalum za swala na kuakhirisha swala baada ya wakati wake ni madhambi makubwa *WALLAAHU-L-MUSTA'AAN.* Kutoka kwa Anas (رضي الله عنه) aliyesema: "Nilimsikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: 'Hii ni swala ya wanafiki, anapokaa akiliangalia jua mpaka likawa katikati ya pembe za shaytaan, kisha ndio husimama kuswali rakaa nne akimkumbuka Allaah kidogo." [Muslim]. Ikiwa hii ni swala ya mnafiki je yule anayepitisha wakati wake kabisa bila ya udhuru wowote?

3 KUACHA SWALA YA JAMAA MSIKITINI KWA WAUME WENYE UWEZO IKIWA NI DAIMA AU MARA KWA MARA

Amri ni kuswali kwa jamaa msikitini. Jamaa ni waajib ila kwa walio na udhuru wakukubalika kisheria. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Yoyote asikiaye mwito (al-adhaan) na baadae asiitikie (kwenda kuswali) basi hana swala ila kwa udhuru ulio sawa" [Ibn Maajah na wengineo kwa isnaad iliyo na nguvu na Ibn Hajar alisema: "Sanad yake ni kulingana na Sharuti za Muslim] Vile-vile Allaah amesema: **"Na inameni pamoja na wanaoinama."** [al-Baqarah-2:43] Katika hadeeth al-Bukhari na Muslim: - *". . .Kisha nitaondoka (baada ya swala kuanza) nende kwa wale wanaume wasiohudhuria swala nizichome nyumba*

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)



(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

zao wakiwa ndani mwazo."

4 KUTOKUWA NA UTULIVU (AT-TUMA'NEENAH) NDANI YA SWALA.

Kwa ujumla jambo hili hufanywa kwa sababu ya ujinga na ni madhambi ya wazi kwa sababu utulivu ni nguzo (ruqn) ya swala ambayo ikosekanapo, swala huwa ni baatil. Hadeeth kuhusu mtu aliyeswali swala yake vibaya ni ushahidi wa wazi kwa hili. Maana ya tuma'neenah ni kuwa yule anayeswali huwa mtulivu katika rukuu (kuinama), 'itidaal (kusimama wima), sujood na kukaa baina ya sijda mbili (juloos) na atakiwa atulie katika kila sehemu mpaka mifupa yote iwe imetulia mahali pake. Na asiharakishe baina ya vituo vya swala mpaka apate utulivu ndani yake na kuipa kila sehemu haki yake. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimwambia yule aliyekuwa akiharakisha swala yake bila ya utulivu: "Rudi ukaswali kwani bado wewe hujaswali". Na kwenye hadeeth ya Rifaa'ah (رضي الله عنه) kuhusu kisa cha aliyeswali vibaya yaendelea: "Kisha apiga takbeer na arukuu na kuweka mikono yake juu ya magoti yake mpaka kila kiungo kimakinike na kutulia. Kisha akasema 'Sami Allaahu liman Hamidah' kisha akasimama wima mpaka kila mfupa ukawa mahali pake.

5 UKOSEFU WA KHUSHOO' (UNYENYEKEVU) NDANI YA SWALA NA MARANGO (EXCESS MOVEMENT) YA ZIADA NDANI YAKE.

Mahali pa khushoo' ni moyoni na ushahidi wake ni utulivu wa viungo na unyenyekevu mbele ya Allaah. Hakika Allaah amemsifu mja wake kwa maneno Yake: **"Ambao kwenye swala zao huwa ni wanyenyekevu."** [al-Muuminoon-23:2] Na vile-vile amewasifu Mitume kwa maneno Yake: **"Bila shaka wao walikuwa wepesi wa kufanya wema, na wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekea."** [al-Anbiyaah-21:90]. Hapana budi kwa viungo vya mja aliye katika swala vitulie na moyo wake umakinike mpaka ikambidi kutuzwa kwa swala yake. Imepokewa kutoka kwa Ammar Ibn Yaasir (رضي الله عنه) aliyesema: "Nilimsikia Mtume (صلى الله عليه وسلم) akisema: 'Hakika mja huswali Swala ambayo haandikiwi chochote (kutokana na Swala hiyo) isipokuwa (1/10) 'Usheri, (1/9) tus'u, (1/8) thumun, (1/7) sub'oo, (1/6) sudus, (1/5) khumus, (1/4) rubu', (1/3) thuluth au (1/2) nusu yake." [Abu Dawood, an-Nasaai na wengineo. Hadeeth swaheeh. Na sababu ya upungufu katika kulipwa kwake ni ukosefu wa khushoo' katika moyo wa yule anayeswali au kwenye viungo vyake.

6 KUMTANGULIA IMAAM KWA KUSUDI KWENYE HARAKATI ZA SWALA AU KUZIKHALIFU HARAKATI ZAKE

Kitendo hichi hubatilisha swala au rakaa' kwa yoyote mwenye ku-rukoo' kabla ya Imaam wake hajaibatilisha rakaa'a yake mpaka aifuatilize baadae na rukoo' nyengine. Na hivyo ndivyo ilivyo katika ruqn zilizobakia za swala. Ni wajib kwa mwenye kuswali kumfuata imaam kikamilifu bila ya kumtangulia au kubaki nyuma katika kila ruqn au zaidi. Abu Daawud na wengineo wamepokea kwa sanad swaheeh kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Hakika imaam atakiwa aandamwe kikamilifu, kwahiyo akipiga takbeer basi pigeni takbeer, na msipige takbeer mpaka apige, na iwapo atarukoo' basi nanyi murukoo' na msirukoo' mpaka arukoo' . . . Asili yake iko katika swaheeh mbili na Al-Bukhari anyo nyingine kama hiyo iliyohadithiwa na Anas. Atakaye sahau au akawa hajui atasamehewa.

7 KUSIMAMA KWA AJILI YA KUKAMILISHA RAKAA' ILIYOKOSEKANA KABLA YA IMAAM HAJAMALIZA KWA UKAMILIFU KUPIGA SALAMU YA PILI.

Imehadithiwa katika swaheeh Muslim kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Musinitangulie mimi katika Rukoo' (kuinama) wala kwenye sujood (kusujudu) wala katika al-insiraaf (kutoka kwenye swala). Wanazuoni wamesema maana ya al-insiraaf ni at-tasleem na inaitwa hivyo kwa sababu mwenye kuswali aweza kuondoka baadae na akaondoka ikipigwa tasleem ya pili tu. Yule ambaye atakiwa kukamilisha akae mahali pake mpaka imaam anapokamilisha swala yake na Allaah ajua zaidi.

8 KUTIA NIA YA SWALA KWA SAUTI KUBWA

Hii ni bid'ah (uzushi), na tumeshataja mbeleni makatazo ya uzushi na hatari zake. Mtume (صلى الله عليه وسلم) hakuwahi kutia nia ya swala kwa sauti ya juu. Ibn al-Qayyim (رحمه الله) alisema katika kitabu chake '*Zaad al-Ma'aad*' au katika '*Al-Hudaa an-Nabawiyy*': "Wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) alipokuwa akisimama kwa ajili ya swala alikuwa akisema: 'Allaahu Akbar' na hakusema chochote kabla ya hayo wala hakutaja nia yake kwa sauti. Wala hakusema, "Nanuiya kuswali kwa ajili ya Allaah, swala kadhaa na kadhaa haliyakuwa nimeelekea Qibla rakaa'a nne kama mfuasi wa Imaam." Wala hakusema: "Nikiitekeleza kwa wakati wake, bila ya kukidhi wala kuiswali katika wakati wa fardh zote kumi zikiwa ni bid'ah na hakuna aliyehadithia hayo kwa sanad swaheeh wala hata sanad dha'eef, wala musnad wala mursal wala neno moja. Hakika hakuna hata hadeeth moja ya Maswahaba wala waliokuja baada yao (taabi'een) wala maimamu wanne."

9 KUTOSOMA AL-FAATIHAH KATIKA SWALA

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

Kusoma al-Faatihah ni nguzo (rukn) na swala ya yeyote asiyeisoma ni baatil. Hii ni kulingana na maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) alivyosema: "Yoyote anayeswali na ikawa ndani mwake (swala hiyo) kukakosekana kusomwa al-Faatihah, basi ni khidaaj (imepotea)- na akarudia (maneno hayo) mara tatu-ni pungufu". [Muslim kutoka kwa Abu Hurayrah]. Vile-vile imehadithiwa katika swaheeh mbili kutoka kwa Ubaadah ibn Saamit (رضي الله عنه) marfoo'an (iliyonasibishwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Swala ni baatil kwani yoyote ambaye hakusoma ufunguzi wa Al-Kitaab." Kwa maneno mengine kutoka kwa 'Ubaadah: "Huenda ikawa mwasoma nyuma ya imaam wenu? Tukasema: "Ndio": Akasema, "Musifanye hivyo illa kwa ufunguzi wa Kitaab (al-Faatiha) kwani swala ni baatil kwa yeyote asiyeisoma. [Ahmad, Abu Daawud, at-Tirmidhi, Ibn Hibaan] Huu ni ushahidi wa faradhi yake kwa Ma'mooma. Usomaji wa Ma'mooma ni lazima au kama kwenye swala zisomwazo kwa sauti kinyume cha ilivyozoeleka kwa muda mrefu. Iwapo kusoma al-Faatihah ni wajibu ni tofauti ya zamani katika maoni baaina ya Wanavyuoni. Ni wajibu au ya kutupwa? Wengi wa Wanavyuoni (al-jumhoor) wanasema yatupwa ingawaje kufanya hivyo ni dhahiri zaidi ya kupatikana makosa na hadhari ya deen. Wengi wa wale wanaosema itupwe wasema hata hivyo ni vizuri kuisoma.

10 KUSOMA QUR'AN KATIKA RUKUU AU KATIKA SOJOOD.

Hili limekatazwa kwa msingi wa hadeeth ya Ibn Abbaas kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Nimekatazwa kuisoma Qur'an katika rukuu na sojood." [Muslim]. Ali (رضي الله عنه) alihadithia kwa kusema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alinikataza mimi nisiisome Qur'an haliyakuwa nimerukoo' au nimesujudu. [Muslim na wengine].

11 KUINUA MACHO MBINGUNI WAKATI WA SWALA AU KUANGALIA KULIA NA KUSHOTO BILA YA SABABU ZAKE

Amma kuhusu kuinua macho, hilo limekatazwa na limebeba tishio la adhabu. Imehadithiwa kutoka kwa Samurah (رضي الله عنه) aliyesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: 'Watu na wawache kuangalia mbinguni wakiwa kwenye swala au hawatorudishiwa macho yao (watapofuka macho)[Muslim].

12 AMA KUANGALIA HUKU NA KULE BILA YA DHARURA NI UPUNGUFU KATIKA SWALA YA MJA

Maadamu mja hajageuza mwili wake wote kuuelekeza kwengine (yaani mbali na qibla). Hatahivyo, iwapo mwili mzima utageuka basi swala itabatilika. Imehadithiwa na Aisha (رضي الله عنها) aliyesema: "Nilimuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu kuangalia kando kando katika swala, akasema: "Ni unyakuzi wa Shaytaan wa kudokoa kutoka kwenye swala ya mja. [al-Bukhari]. Vile-vile at-Tirmidhee amepokea hadeeth iliyo swaheeh: "Tahadhari na kuzunguka na kuangalia huku na huku katika swala kwa sababu huondosha umakinifu". Na kuna ahaadeeth nyengine zinazohusiana na swala.

13 KUKAA KITAKO (AL-IQ'AA) WAKATI WA SWALA NA KUSUJUDU KWA VISUKUSUKU (*AL-IFTIRAASH*) KATIKA ARDHI.

Al-iqaa' imekatazwa kama ilivyohadithiwa na Abu Hurayrah (رضي الله عنه) aliyesema: Rafiki yangu mpendwa alinikataza mimi mambo matatu: Amenikataza kudoma kama jogoo (kudara sujood kwa haraka) kukaa kitako kama mbwa, na kuangalia huku na huku kama mbweha. Ahmad na wengineo na isnaad yake ni hasan kwa mujibu wa al-Mundhiri na al-Haithami. Mtume (صلى الله عليه وسلم) alimkataza mtu kuitandaza mikono yake kwenye ardhi kama mnyama wa kuwinda. Katika kuieleza kwa mukhtasari hadeethi ya Aisha (رضي الله عنها) iliyopokewa na Muslim na pia at-Tirmidhee, Ahmad na wengineo kutoka kwa Jaabir (رضي الله عنه) marfoo'an (yenye kunasibishwa kwa Mtume (صلى الله عليه وسلم)): "Anaposujudu mmoja wenu, basi na ajinyo-oshe sawa (straight) na asiitandaze mikono yake kama kikao cha mbwa.

14 KUVAA NGUO NYEMBAMBA (YENYE KUONYESHA NDANI) AMBAYO HAITOSHELEZI KUSITIRI AUWRAH (SEHEMU ZA SIRI)

Hili ni lenye kuharibu swala kwa sababu kusitiri 'awrah ni katika shuruti za swala iliyo swaheeh. Uchi wa mwanamume ni – kulingana na kilicho swaheeh - baina ya kitovu na magoti. Na pia ni lazima afunike mabega yake, au japokuwa moja kulingana na maneno ya Allaah (سبحانه وتعالى): "**Enyi wanaadamu! Chukueni mapambo yenu wakati wa kila swala.**" [Al-A'raaf-7:31].

Yatosheleza kuvaa nguo moja kufunika 'awrah kulingana na hadeeth ya 'Umar Ibn Salamah (رضي الله عنه): Alimuona Mtume (صلى الله عليه وسلم) akiswali kwa nguo moja (thawb) nyumbani kwa Umm Salamah, akiwa amejitanda nayo (kuizungusha mwilini) ncha zake mbili [al-Bukhari & Muslim].

Ibn Qudaamah (رحمه الله) amesema: "Ni wajibu kujifunika vya kutosha ili kuficha rangi ya ngozi, kwani iwapo nguo ni nyembamba kiasi cha kwamba huwenda ngozi ikaonekana kwa nyuma mpaka weupe au wekundu (wa ngozi) ukatambulika, basi kuziswalia nguo hizo hakujuzu ikiwa hakutopatikana kujisitiri huko.

15 MWANAMKE ASIYEJISITIRI KICHWA CHAKE KWA *KHIMAAR* NA

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

ASIYEJISITIRI MIGUU YAKE KATIKA SWALA

'Awrah ya mwanamke katika swala ni mwili wake wote illa uso, wala hakuna ubaya akifunika uso wake kutokana na mapito ya wanaume au mfano wake. Ni wajibu kwake kuvaa khimaar ambayo ni kitambara cha kufunika kichwa pamoja na sehemu nzima ya kifua chake (yakiwemo matiti). Haya ni kulingana na matamshi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Allaah haikubali swala ya mwanamke awezae kupata heidh (damu) mpaka awe amevaa khimaar." {Ahmad na wakusanyaji wa vitabu sita vilivyo swaheeh isipokuwa an-Nasaai na imeswahihishwa na Ibn Khuzaymah na wengineo. Ni wajib pia afunike juu ya miguu yake kulingana na hadeeth: "Mwanamke mzima ni awrah" [at-Tirmidhi kwa sanad swaheeh] na pamoja na maana sawa ni hadeeth iliyopokewa na Maalik na Abu Daawud na wengineo kutoka kwa Muhammad Ibn Said Ibn Qunfudh kutoka kwa mamake aliyemuuliza Umm Salamah (رضي الله عنها), mke wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu nguo inayompasa kuswalia mwanamke. Akajibu: "Atakiwa avae khimaar na Shimizi ndefu iliyo pana, tena ifiche mpaka sehemu za juu ya miguu yake. Pia katika hadeeth yake Ummu salamah: "Iteremshe chini kwa kiasi cha pima moja.

KUPITA MBELE YA MTU ANAYESWALI, EMMA AKIWA NI IMAAM AU MWENYE KUSWALI PEKE YAKE NA KUWARUKA WATU WAKATI WA KHUTBAH YA IJUMAA

Ni dhambi kwa mtu kupita mbele ya mtu anayeswali. Ikiwa anaeswali hana Sutrah, basi na pakisiwe (mahali pa sutrah) kuwa ni pale anaposujudu. Kwahiyo mwenye kupita na apite kando ya mahala hapo pa kusujudu. Kama ilivyo katika al-Bukhari na Muslim kutoka kwa Abu Juhaim Ibn Haarith (رضي الله عنه) aliyesema: "Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: 'Lau angelijua mwenye kupita mbele ya mwenye kuswali madhambi yaliyo juu yake ingekuwa kusimama arubaini ni bora kwake kuliko kupita mbele ya mwenye kuswali. (Abu an-Nadr asema, "sikumbuki vizuri iwapo alisema siku arubaini, miezi au miaka.')"

Yule anayewatenganisha watu wakati wa khutbah ya ljumaa huwadhuru watu kutokana na kuchelewa kwake kwa swala kulingana na maneno ya Al-Mustafah (صلى الله عليه وسلم): "Keti chini hakika wewe umesababisha madhara na umechelewa." [Ahmad na wengineo]. Kuwatenganisha watu imeharamishwa. Anayeingia msikitini na akae palipo na nafasi, isipokuwa iwapo ataona nafasi ya wazi ndipo awezapo kuiindea na kukaa.

17 KUTOTAMKA *TAKBEERATUL -IHRAAM* (*TAKBEER* YA UFUNGUZI) UINGIAPO KWENYE JAMA'AH WAKATI IMAAM AKIWA KATIKA RUKOO'

Haya ni makosa makubwa kwa kuwa takbeeratul-ihraam ni nguzo (ruqn) ya swala ambayo ni lazima itamkwe na mwenye kuingia katika swala anaposimama kwa ajili ya kuswali na kisha amuunge Imaam katika rukoo'. Kuitamka takbeer (al-Ihraam) na kisha kufuatiza takbeer nyengine kabla ya kwenda kwenye rukoo' ni bora na kamilifu zaidi. Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alihadithia kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akipiga takbeer anaposimama kwa ajili ya kuswali kisha akipiga takbeer anaporukoo'.

18 KUTOMFUATA IMAAM (KWA KUWA SAWA NAE) KWENYE SWALA UNAPOINGIA KWA KUCHELEWA UKAMKUTA IMAAM AMEKAA AU AMESUJUDU

Yapendekezwa na ndio sawa kumuunga Imaam akiwa katika hali yoyote, iwapo itakuwa ni sajdah au sehemu nyengine iwayo. Imepokewa na Abu Daawud na wengineo kwa sanad swaheeh kuwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Ukija kwenye swala na ukatupata tuko kwenye sujood basi nawe pia sujudu nasi." Kwa mja kucheleweshe hilo ni kujizuia na kitendo cha ibada akipendacho Allaah". Ali Ibn Abi Twaalib na Mu'aadh Ibn Jabal (رضي الله عنهم) wote walisema: Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "Aingiapo kwenye swala mmoja wenu akamkuta Imaam katika kitendo kiwacho, basi na amfuate Imaam katika kitendo chake. [at-Tirmidhi kwa sanad dha'eef lakini yakubaliana na hadeeth iliyopita. Pia yatiliwa nguvu na hadeeth iliyopokewa na Abu Daawud kutoka kwa Mu'aadh (رضي الله عنه) aliyesema: 'Sikuwahi kumuona (Imaam) akiwa katika kitendo chochote illa nami nilimuunga katika kitendo hicho. Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "Hakika Muadh amefanya kitendo kizuri kwenu nyinyi, basi fanyeni kama hivyo."